

# Mpango wa Familia Zilizofanikiwa

Julai 2003

Mpango wa Familia zilizofanikiwa una huduma za familia zenye mapato ya chini pamoja na zifwatazo:

- Msaada wa kifedha, unaojulikana pia kama Msaada wa Muda wa Familia (TAF)
- Huwasaidia watu wazima na shida zao za kupata kazi
- Hutoa huduma ya msaada ya mafunzo ya kazi, shughuli za kazi, na elimu

Mpango huu husaidia familia kuongeza ustadi wao, kuongeza uwezo wao, na kuweka watoto manyumbani mwao.

Ili kupokea msaada kutoka kwa Familia Zilizofaulu, familia lazima iwe na mtoto mmoja nyumbani aliye na umri wa chini ya miaka 18. Pia mtoto anaweza kuwa hajazaliwa. Mtoto anaweza kuishi na mzazi au jamaa. Pia mtoto anaweza kuishi na mtu aliyetajwa na korti amlee mtoto huyo, kama vile mlezi, mhifadhi, au mtunzaji.

Familia lazima ziwe na mapato na rasilimali za chini. Mapato ya watoto wote na wazazi wao nyumbani uhesabiwa. Aina zingine za mapato na rasilimali hazihesabiwi, kama hizi zifwatazo:

- Nyumba ambayo familia inaishi
- Mali chini ya \$2,000
- Magari
- Fanicha, vitu vya kibinafsi, na vifaa vingine
- \$90 pamoja na asilimia 40 ya mapato

Familia zinaweza kupata msaada wa kifedha wanapokuwa wakitafuta kazi maadamu wanafikia mahitaji ya mpango. Hii ni pamoja na kushirikiana na mahitaji ya Mpango wa Msaada wa Watoto. Familia zinaweza kupata TAF kwa miezi 60 tu katika maisha yao. Familia zinazopata TAF pia zinapata manufaa ya matibabu na zinaweza kupata ulezi wa mtoto.

Viwango vya manufaa ya kifedha vinategemea mapato ya familia. Kiwango cha mufaa pia kinategemea jimbo ambalo familia inaishi. Chati iliyo hapo chini inaonyesha manufaa ya juu kabisa ya kifedha ambayo familia inaweza kupokea.

Malipo ya Msaada wa Kifedha				
Ukubwa wa Familia	Mkoa wa Mashambani	Mashamba ya Gharama ya Juu	Mikoa Yenye Watu wengi	Gharama ya juu-Watu Wengi
1	\$224	\$229	\$241	\$267
2	\$309	\$314	\$326	\$352
3	\$386	\$391	\$403	\$429
4	\$454	\$459	\$471	\$497
5 au zaidi	Ongeza \$61 kwa kila mtu wa ziada			

Familia zinaweza kupata aina zingine za huduma za misaada ambazo zinapunguza vizuizi vyao vya kufanya kazi. Familia zinaweza kupokea huduma hizi za msaada wanapokuwa wakipata msaada wa kifedha na pia mwaka baada ya kuwacha kupokea msaada wa kifedha. Familia zinaweza kupokea huduma na misaada tofauti, pamoja na zifwatazo:

Huduma za ulemavu wa kusoma, shida za madawa au pombe, au mzozo wa kinyumbani  
Huduma za kusaidia kusoma na kuhesabu  
Huduma za afya ya kiakili  
Matibabu ya kimwili  
Usaidizi wa kuvumiliana na ulemavu  
Usaidizi wa kupata na kutunza kazi  
Usaidizi wa uzazi  
Usaidizi wa kupata meno bandia, miwani, vifaa vya kusaidia kusikia  
Mafunzo ya kazi  
Usaidizi wa kupata GED au kujifunza Kiingereza  
Ujuzi wa kazi  
Usaidizi wa kufika maeneo ya kazi  
Mavazi  
Msaada wa mahitaji muhimu  
Gharama ya kuhama kunaohusina na kazi

Watu wazima chini ya umri wa miaka 60 lazima wafanya mojawapo ya yafwatayo ndiposa kupokea msaada wa kifedha wa familia yao:

Wawe kazini au katika shughuli za kikazi  
Wawe katika mipango ya kusaidia kupunguza vizuizi vya kufanya kazi  
Wawe wanamlea mtoto chini ya umri wa miaka 12  
Wawe wanamlea mmoja wa kaya ambaye ni mlemavu

Watu ambao hawahitajiki kupata kazi au kuwa katika shughuli za kikazi wanaweza kuuliza huduma.

### Maombi

Bonyeza hapa ili kufikia maombi ya huduma zetu.

Kwa huduma zingine, au kupata Ofisi ya Jamii na Urudishaji au Eneo la Kufikia lililo karibu na wewe, tumia viungo vilivyo mwisho wa ukurasa huu.

Rudi kwa Gombo kaya ya EES

Ukurasa Ulisasishwa: Septemba 16, 2004